



Alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- anapopiga chafya anaweka mkono wake au nguo yake juu ya kinywa chake, na anapunguza sauti yake

Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Alikuwa Mtume -
Rehema na amani ziwe juu yake- anapopiga chafya anaweka mkono wake au nguo yake
juu ya kinywa chake, na anapunguza sauti yake.

[Sahih]

Alikuwa rehema na amani ziwe juu yake anapopiga chafya: Jambo la kwanza: Anaweka
mkono wake, au nguo yake juu ya kinywa chake; Kisije kutoka kinywani mwake au puani
mwake chochote kitakachomuudhi aliyekaa naye. Jambo la pili: Anashusha sauti yake na
wala hainyanyui.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3317>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

